

**KIWANGO CHA UZINGATIAJI WA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU
ZINAZOSIMAMIA RASILIMALI WATU CHAONGEZIKA KATIKA
UTUMISHI WA UMMA.**

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

Kiwango cha uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma kimeongezeka kutoka 52% kwa mwaka 2005/2006 hadi kufikia kiwango cha 70% kwa mwaka 2007/2008.

Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma, Bibi Cecilia Shirima ameyasema hayo katika taarifa iliyotolewa na Katibu Msaidizi wa Idara ya Utumishi Serikalini, Tume ya Utumishi wa Umma Bibi Neema Tawale katika Ziara ya Tume ya Utumishi wa Umma inayofanyika katika Mkoa wa Dodoma na Singida.

Kamishna Shirima ameyataja madhumuni ya ziara hiyo kuwa ni kujitangaza kwa Tume ya Utumishi wa Umma ili wadau wake waweze kuifahamu Tume, kutoa fursa kwa wadau kutoa mrejesho wa utendaji wa kazi za Tume na kuwaelimisha wadau wa Tume Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8, mwaka 2002 kama ilioyorekebishwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 18, 2007.

Bibi Shirima ameyataja maeneo ambayo kiwango cha uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu kimeongezeka kuwa ni pamoja na ajira, likizo, upimaji wa wazi wa utendaji kazi (OPRAS) na nidhamu. Kuwepo kwa ongezeko la uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu kunaashiria kuwepo kwa ongezeko la uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma. Uelewa huo umeonekana kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu baada ya Tume ya Utumishi wa Umma kufanya ukaguzi wa Rasilimali watu katika Mamlaka mbali mbali za Ajira na Nidhamu katika Utumishi wa

Umma. Miongoni mwa Taasisi zilizokaguliwa ni pamoja na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Kamishna Shirima amefafanua kuwa ongezeko la uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu unatokana na jitihada ambazo zimefanywa na Tume ya Utumishi wa Umma kwa kufanya Semina na Mikutano ya kazi na wadau mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Aidha, amesema kuwa ongezeko la uzingitaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu umetokana pia na uandaaji na usambazaji wa Rejea za Sera, Sheria, Kanuni na Nyaraka mbalimbali kuhusu masuala ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Miongozo ya Ajira na Nidhamu na Rufaa, maelezo mahsusi ya namna ya kuendesha Kamati za Uchunguzi katika Utumishi wa Umma, Vipeperushi, Majarida, kutoa makala katika magazeti na vipindi vya Redio. Tume ya Utumishi wa Umma inaendelea na utoaji wa elimu kwa wadau wake ili kuhakikisha kuwa wadau wake wamefahamu kikamilifu Sheria na Utumishi wa Umma Na. 8 mwaka 2002 kama ilivyorekebisha na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 18, mwaka 2007.

Katika Mkoa wa Dodoma na Singida Tume ya Utumishi wa Umma imefanya Ziara zake katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Taasisi za Serikali na Halmashauri na Manispaa za Wilaya. Aidha, Tume ya Utumishi wa Umma inafanya Ziara hizo katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Kagera na Kilimanjaro. Baada ya Ziara hizo ambazo zinatarajiwa kufikia mwisho wake tarehe 27 Novemba, 2009 Tume itaendelea tena na Ziara hizo katika Mikoa mwingine.

Iwapo una maoni au masuala tafadhali tuandikie:

Katibu,

Ofisi ya Rais,

Tume ya Utumishi wa Umma,

S.L.P. 9143,

DAR ES SALAAM.